



MAKOSA YA KIMATAMSHI YANAYOFANYWA NA WANAFUNZI WA LIBYA WANAPOJIFUNZA KISWAHILI

Ibrahim Elhadi Mohamed Lehmedi

Idara ya lugha na taaluma za kiafrika, kitivu cha sanaa, chuo kikuu cha sebha, Libya

Keywords:

Athari
Irabu
Kimatamshi
Makosa
Mfuatano
Sauti

ABSTRACT

Utafiti huu unalenga kuchanganua na kuchunguza makosa ya kimatamshi yanayofanywa na wanafunzi wa Libya wanapojifunza kiswahili. Ili kutekeleza kazi hii, nadhariatete zilijadili, ikiwa ni pamoja na kuwa chanzo cha makosa na matatizo hayo ni kutokana na sababu kadhaa, zikiwemo tofauti za mfumo wa kifonolojia baina ya lugha ya Kiarabu na Kiswahili, Matamshi ya sauti zinazopatikana katika Kiswahili na hazipatikani katika Kiarabu, Athari ya matamshi ya sauti za Kiarabu zinazopatikana katika maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu pamoja na matamshi ya mfuatano wa mfululizo wa irabu mbalimbali.

Utafiti huo ulifanya kwa idadi ya wanafunzi wa idara ya lugha ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Sebha ili kujua aina na ukubwa wa mateso, kujua sababu za matatizo na makosa haya, na kutafuta ufumbuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wa Libya, na kuweka mapendekezo ambayo kuchangia katika kutatua matatizo haya.

أخطاء النطق التي تواجه الطلاب الليبيون أثناء تعلمهم اللغة السواحلية

ابراهيم الهايدي محمد لحميدي

قسم اللغات والدراسات الأفريقية، كلية الآداب ، جامعة سبها، ليبيا

الكلمات المفتاحية:

أثر
أخطاء النطق
تلاحق
صوت
محرك

الملخص

هذا البحث يهدف لتحليل ودراسة أخطاء النطق التي يرتكبها الطلاب الليبيين أثناء تعلمهم اللغة السواحلية. وللقيام بهذا العمل تمت مناقشة الفرضيات التي منها ان سبب هذه الأخطاء المشاكل راجع الى عدة اسباب من ضمنها اختلاف النضام الفونولوجي بين اللغتين العربية والسواحلية، نطق الأصوات الموجودة في اللغة السواحلية وغير موجودة في العربية، تأثير نطق الأصوات العربية الموجودة في الكلمات السواحلية ذات الأصل العربي كذلك نطق تلاحق عدد متسلسل من الحروف المتحركة. تم اجراء الدراسة على عدد من طلاب قسم اللغة السواحلية جامعة سبها للوقوف على نوع وحجم المعاناة لتعلم اسباب هذه الأخطاء المشاكل ومن تم ايجاد الحلول لهذه المشاكل التي يعانيها الطالب الليبيين وطرح العديد من المقترنات التي من شأنها ان تسهم في حل هذه المشاكل.

1. UTANGULIZI

Kiswahili ni lugha mojawapo kati ya lugha za Kiafrika, na ambayo hivi sasa imepata umaarufu mkubwa. Kwa mujibu wa Greenberg (1967) lugha hii imo katika mbari kubwa ya lugha za Kinija-Kordofani. Chini ya mbari hii kubwa kuna familia kubwa ijulikanayo kama Nija-Kongo, ambayo chini yake kuna familia ndogo ijulikanayo kama Benue Kongo. Lugha za Ki-bantu, Ki-Swahili kikiwemo, ziko chini ya familia hii ya Benue-Kongo.

Katika uainishaji wake, Guthrie (1970) anakiingizia Kiswahili katika kanda G¹⁰ kundi G⁴². Idadi ya wazungumzaji wake wanakadiriwa kuwa zaidi ya milioni 60 (Massamba na wenzie 2001).

Lugha ya Kiswahili imekuwa ni somo mojawapo katika shule za Libya. Mnamo mwaka 1984 kulifunguliwa Idara ya Lughya za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Sebha, nchini Libya. Idara ilipewa jukumu la kufundisha lugha za Kiswahili Kihausa na Kifolani. Kuanzia mwaka 2000 lugha ya Kiswahili imeanza kufundishwa pia katika shule za matayarisho ya sekondari nchini Libya. Hii ina maana kwamba viwango vya elimu ya Kiswahili nchini Libya ni vya namna mbili, kiwango cha shule za matayarisho ya sekondari na kiwango cha Vyuo Vikuu.

Katika kujifunza au kufundisha lugha yoyote ya kigeni mwanafunzi au mwaliimu hukumbana na matatizo ambayo yanahitaji kuzingatifa

*Corresponding author:

E-mail addresses: ibr.lehmedi@sebhau.edu.ly

na kuchunguzwa kwa makini. Matatizo ya kujifunza lugha ya pili yanatofautiana kulingana na umri wa mwenye kujifunza na mazingira ya kuishi wakati wa kujifunza lugha hiyo (taz. Besha 1983). Pia matatizo haya yanatofautiana toka lugha moja hadi nyingine. Kwa mfano inadhihirika kwamba ni rahisi kwa Mfaransa kujifunza Kitaliano au Kihiispania kuliko kujifunza Kiingereza au Kijerumani. Aidha Mfaransa anapata matatizo makubwa zaidi anapojifunza lugha tofauti kabisa na lugha za familia ya lugha yake, kama vile Kiarabu au Kichina. Kwa upande mwingine ni rahisi kwa Mwarabu kujifunza Kifarsi na Kiurdu lakini anapata shida zaidi katika kujifunza lugha kama Kiingereza au Kichina (Alhadidi 1978).

Baadhi ya matatizo hayo ni kama yale ya kimofolojia. Kwa mfano, inawezekana mwanafunzi wa lugha ya Kiswahili ambaye lugha yake ya kwanza ni Kiarabu akapata matatizo ya kuzingatia dhana ya ngeli ambayo haimo katika lugha yake. Kwa upande mwingine mwanafunzi wa lugha ya Kiarabu ambaye lugha yake ya kwanza ni Kiswahili atapata matatizo ya kuzielewa nomino za Kiarabu ambazo zimegawanyika katika makundi ya kijinsia. Mfano wa wazi hapa, ni ule unaohusu wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kiarabu kukabiliwa na tatozo la kuzielewa njeo za Kiswahili ambazo ni : *a-, hu-, -na-, -me-, -li-* na *-ta-*. Hii ni kwa sababu katika lugha ya Kiarabu kuna njeo tatu tu: *na, li na ta*.

Matatizo mengine ni ya kisintaksia. Kwa mfano, inawezekana mwanafunzi wa Kiarabu akapata matatizo ya kuzingatia dhana ya miundo ya virai mbalimbali katika Kiswahili. Mfano mzuri ni wa miundo ya virai nomino ambapo Kiswahili kinakuwa na mfuatano wa *Nomino . Kionyeshi* wakati katika lugha ya Kiarabu mfuatano wake ni *Kionyeshi . Nomino*.

Ingawa kuna aina hizo kadhaa za matatizo, katika utafiti huu tutajibana katika matatizo ya kimatamshi peke yake.

2. Nadhariate

Wanafunzi wa Kiarabu ni kundi mojawapo la wageni ambao hukabiliwa na matatizo mbalimbali mionganoni mwa matatizo haya ni makosa ya kimatamshi ambayo yanatokana na sababu zifuatazo:

(i) Lugha ya Kiarabu na lugha ya Kiswahili ni lugha zinazotoka katika familia mbili tofauti za lugha. Ama kuhusu hili Kihore (1984) anasema:

Lugha hizi mbili zinatofautiana katika mambo mengi hazikaribiani hata kijamii. pamoja na maingiliano hayo yote Kiswahili na Kiarabu zimedumu kujitambulisha kama lugha tofauti

Lugha ya Kiarabu inatokana na familia kuu ya Ki-Afro Asia wakati kama tulivyokwishaona lugha ya Kiswahili inatokana na kundi au familia Kuu ya Kinija- Kordofani (Greenberg 1963); (Heine 1979). Kwa misingi hiyo lugha hizi mbili ni lazima zitofautiane.

(ii) Kuna tofauti za kifonolojia baina ya lugha ya Kiarabu na lugha ya Kiswahili. Kiswahili kinazingatia taratibu na kanuni za lugha za Kibantu (Besha 1983; Basha 1994; Massamba 2001) wakati Kiarabu kinazingatia taratibu na kanuni za lugha za Kisemiti (Aniss 1965).
 (iii) Wanafunzi wa Kiarabu huathiriwa na lugha yao ya kwanza wanapojifunza Kiswahili. Kuhusu hoja hii, Besha (1983) anasema:

..... Fonolojia ya lugha ya mwanafunzi ya awali itakuwa imemkaa sana hivyo atajaribu kulinganisha sauti za lugha ngeni na zile sauti za lugha yake, na mara nyngi atashindwa kuweka tofauti za matamshi ambazo ni muhimu katika lugha ngeni lakini hazipatikani katika lugha yake

Kwa kawaada athari za lugha ya awali huathiri sana lugha ya pili (Gurrey 1959; Haji 1983)

3. Malengo Ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu ni kuchunguza na kutoa utatuza kwa makosa ya kimatamshi yanayofanywa na wanafunzi wa Kiarabu wanapojifunza Kiswahili. Ili tuweze kufikia azma hiyo itafaa tuukabili utafiti wetu kwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Makosa yatokanayo na utamkaji wa sauti hupatikana katika lugha ya Kiswahili na hazimo katika lugha ya Kiarabu.
 (ii) Makosa yatokanayo na athari za utamkaji wa sauti za Kiarabu

ambazo hazimo katika lugha ya Kiswahili (au ambazo zina asili ya Kiarabu).

(iii) Makosa yatokanayo na utamkaji wa mfuatano wa irabu mbalimbali.

4. Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unatarajiwa kuwa na faida kwa wadau wote wenye kujifunza na kufundisha Kiswahili kama lugha ya pili. Kukamilika kwa uchunguzi huu kutaoa taarifa muhimu kuhusu makosa ya kimatamshi yanayofanywa na wanafunzi wa Kiarabu wanapojifunza Kiswahili sanifu. Halikadhalika, utafiti utawasaidia walimu na wanafunzi wa Kiarabu wanaofundisha na kujifunza Kiswahili kuweza kuyaewa matatizo hayo.

5. Mapitio ya Kazi

Kutokana na matatizo mbalimbali ambayo huwakabili watu wanaojifunza lugha za kigeni wataalamu kadha wa ufundishaji wa lugha kama lugha ya pili wamewahi kuandika na kujaribu kuyabainisha baadhi ya matatizo hayo.

Kuhusu uzoefu wa ufundishaji wa lugha ya Kifaransa Magoti (1980) anasema kwamba wanafunzi wa Tanzania huchukua muda mrefu kudhibiti baadhi ya sauti za Kifaransa. Anahitimisha kwamba hii hutokana na athari ya Kiswahili.

Kassulamemba (1977) alichunguza utamkaji wa baadhi ya irabu za Kiingereza na wanafunzi wa Tanzania wanaojifunza Kiingereza. Anasema kwamba wanafunzi wengi wana matatizo ya kutamka maneno ya Kiingereza. Utafiti wake ulipendekeza kwamba makosa hayo yanatokana na athari za lugha yao ya kwanza, mwingiliano wa lugha na mwelekeo hasi kuhusu lugha ya Kiingereza.

Ama kuhusu Kiarabu, Rawhia (1984) katika utafiti wake wa matatizo wanayopata wanafunzi wa Kiingereza wanapojifunza Kiarabu, anasema kwamba matatizo yanayowakabili walimu na wanafunzi yanatokana na lugha yenye. Lugha ya Kiarabu si rahisi kwa wazungumzaji wazima wa Kiingereza kujifunza. Hawa kwa kawaada wanakabiliwa na matatizo mbalimbali yanayohusu fonolojia na sarufi ambayo siyo sawa na Kiingereza. Ama kuhusu irabu fupi na ndefu hakika ni tatozo. Kiarabu kina irabu tatu fupi [a], [i], [u] na tatu ndefu [a:], [i:], [u:]. Pamoja na hivyo Kiarabu kina konsonanti ambazo hazimo katika Kiingereza.]

Kwa hakika wanaisimu hawa wote wamebainisha matatizo ya ruwaza za namna anuwai. Wa ama, maandishi yote hayo yamegusia matatizo ya kila aina. Lakini kama tulivyokwishesema sisi tutajibana katika matatizo ya kifonolojia tu. Jambo la msingi kusema hapa ni kwamba katika maandishi yaliyopitiwa hapa juu hapana mahali ambapo nadharia toshelevu ya fonolojia imetumika kueleza matatizo haya; maoni yaliyotolewa yamekuwa ni ya kijuu juu tu.

Aidha mpaka sasa sijawahi kuona wataalamu ambao wamewahi kufanya utafiti kuhusu matatizo ya matamshi wanayopata wanafunzi wa Kiarabu wanapojifunza Kiswahili sanifu. Kwa hivyo iko haja ya kufanya utafiti ili kuonyesha matatizo hayo na kuchunguza vyanzo vyake. Utafiti huu unatumia kanuni na taratibu bayana za kifonolojia kuonyesha ni vipi zinakuwepo "athari" hizo za lugha ya kwanza katika lugha ya pili ya mzungumzaji.

6. UCHAMBUZI WA DATA

Ili kuweza kuelewa kwa undani matatizo na makosa hayo ya kimatamshi inabidi tuanze na nadhariate kwamba makosa ya kimatamshi yanayofanywa na wanafunzi wa Kiarabu wanapojifunza Kiswahili sanifu yanatokana na tofauti na athari za kifonolojia za lugha hizi mbili.

Katika kuchunguza matatizo hayo ingefaa tukayagawa katika makundi matatu, kwanza, ni makosa yatokanayo na utamkaji wa sauti ambazo hupatikana katika lugha ya Kiswahili lakini hazimo katika lugha ya Kiarabu. Pili, ni makosa yatokanayo na athari za utamkaji wa maneno yenye asili ya Kiarabu; yaani maneno yenye sauti ambazo hupatikana katika lugha ya Kiarabu lakini hazimo katika lugha ya Kiswahili. Tatu, makosa yatokanayo na utamkaji wa

maneno yenye mifululizo wa irabu mbalimbali ambayo hukubalika katika lugha ya Kiswahili lakini haikubaliki katika lugha ya Kiarabu.

6.1 Makosa yatokanayo na utamkaji wa sauti ambazo hupatikana katika lugha ya Kiswahili lakini hazimo katika lugha ya Kiarabu

Kama lugha ya Kiswahili ina jumla ya sauti sita ambazo hazipatikani katika lugha ya Kiarabu. Sauti hizo ni konsonanti sita, yaani [p, v, ch, ny, ng', g].

Katika utafiti wa uwandani tuliofanya kwa wanafunzi yaliyotajwa, tuliwapa maneno na sentensi zenyne maneno yenye asili ya Kiarabu. Hebu tuangalie maneno yaliyotumika katika zoezi hili:

| neno | sauti iliyolengwa |
|---------|-------------------|
| papi | p |
| vua | v |
| gari | g |
| chai | ch |
| nyanya | ny |
| ng'ombe | ng' |

Aidha sentensi zilizotumika katika utamkaji wa sauti zilizoorodheshwa hapo juu ni hizi zifuatazo:

1. Pengine baba atanipa kitabu kesho.
2. Fundi alipaka nyumba yetu rangi.
3. Leo tumevua samaki wengi.
4. Mtoto amefua nguo zake.
5. Tulijenga nyumba ya chumba kimoja shambani.
6. Chama cha siasa kilishinda.
7. Nyanya ni kiungo kitamu sana.
8. Nyinyi mnaalikwa nyumbani kwetu.
9. Jana baba alichinja ng'ombe.
10. Katika lugha ya Kiarabu hakuna ving'ong'o.
11. Mteja alinunua gundi nyingi.
12. Unaweza kuzungumza Kiswahili kwa kiwango gani?

| Sauti | | neon | Matamshi ya Kiswahili | Matamshi ya wanafunzi | | |
|-------|---------|---------|-----------------------|-----------------------|----------|-------|
| P | papai | [papai] | [papai] | [papai] | [babai] | Jumla |
| | | | | 5 % | 95% | 100% |
| V | vua | [vua] | [vua] | [vua] | [fua] | Jumla |
| | | | | 15% | 85% | 100% |
| G | gari | [gari] | [gari] | [gari] | --- | Jumla |
| | | | | 100% | 0% | 100% |
| Ch | chai | [tʃai] | [tʃai] | [ʃai] | --- | Jumla |
| | | | | 60% | 40% | 100% |
| Ny | nyanya | [napa] | [napa] | [napa] | --- | Jumla |
| | | | | 100% | 0% | 100% |
| ng' | ng'ombe | [ŋombɛ] | [ŋombɛ] | [ŋombɛ] | [ŋgumbi] | Jumla |
| | | | | 0% | 100% | 100% |

Matokeo ya utamkaji wa wanafunzi.

6.2 Makosa yatokanayo na athari za utamkaji wa sauti za Kiarabu ambazo hazimo katika lugha ya Kiswahili (au ambazo zina asili ya Kiarabu).

Lugha ya Kiarabu ina sauti tisa ambazo hazipatikani katika lugha ya Kiswahili. Sauti hizo ni [፻, ፻, ፻, ፻, ፻, ፻, ፻, ፻, ፻, ፻, ፻, ፻, ፻]. Aidha lugha ya Kiswahili ina maneno mengi ambayo yamekopwa kutoka lugha ya Kiarabu (taz. Bosha, I. 1993:39). Maneno hayo yalikopwa yamechukua utaratibu na kanuni za lugha ya Kiswahili; yaani, baadhi ya vitamkwa vimedondoshwa au vimebadilishwa. Kwa hiyo maneno hayo hayatamkiki kama yanavyotamkwa katika Kiarabu.

13. Mama alimchemshia mgeni maji.
14. Rangi ya bendera yetu ni kijani.
15. Wanafunzi wanapenda kuogelea wakati wote.

Wanafunzi walipewa maneno na sentensi za kusoma, ili kujua Matatizo yatokanayo na sauti za Kiswahili ambazo hazimo katika lugha ya Kiarabu. Hebu tuangalie matokeo ya utamkaji wao.

Sauti [p]: Matokeo ya utamkaji wa sauti hii yalionyesha kwamba wanafunzi wengi wana shida ya kuitamka sauti hii; ni mwanafunzi mmoja tu ambaye aliweza kuitamka sauti hii kwa usahihi, wakati wanafunzi kumi na tano walitamka kama sauti [b]. Kwa mfano, neno [papai] walilitamka [babai].

Sauti [v]: Ni wanafunzi wawili tu ambao waliweza kuitamka sawasawa. Sauti hii ilitamkwa kama sauti [f] na wanafunzi kumi na nne. Kwa mfano, neno [vua] walilitamka [fua].

Sauti [g]: Kutokana na utamkaji wa wanafunzi ilioneckana wazi kwamba hawakuwa na shida yoyote katika kuitamka sauti hii. Yaani wanafunzi wote kumi na sita waliweza kuitamka barabara.

Sauti [ch]: Wanafunzi wa nane waliweza kuitamka sauti hii sawasawa. lakini wanafunzi wanane waliobaki walitamkwa kama sauti [sh]. Kwa mfano, neno [tʃai] walilitamka [ʃai].

Sauti [ny]: Sauti hii ilitamkwa sawasawa na wanafunzi wote kumi na sita.

Sauti [ng']: Sauti hii iliwateranisha wanafunzi wote kumi na sita; mara nyingi walitamkwa kama ng. Kwa mfano, neno [ŋombɛ] walilitamka [ŋgumbi]

Matokeo ya utamkaji wa sauti ambazo hupatikana katika lugha ya Kiswahili lakini hazimo katika lugha ya Kiarabu kwa kundi hili yanaweza kuelezwaa kwa kutumia Jedwali lifuatalo:

Katika utafiti wa uwandani tuliofanya kwa wanafunzi yaliyotajwa, tuliwapa maneno na sentensi zenyne maneno yenye asili ya Kiarabu. Hebu tuangalie maneno yaliyotumika katika zoezi hili:

| neno lenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili | imetokana na | sauti iliyoyotamkwa |
|--|--------------|---------------------|
| maařifa | [mařifa] | ‘ (ع) |
| tarehe | [tari:xi] | kh (خ) |
| sifuri | [šifr] | š (ص) |
| maradhi | [marađi] | d (ض) |

| | | |
|-----------------|------------|--------------|
| <u>hewala</u> | [hawa:la] | h (ح) |
| <u>kabila</u> | [qabi:la] | q (ق) |
| <u>hatari</u> | [xatar] | t (ط) |
| <u>swali</u> | [su:?!] | ? (ء) |
| <u>nadharia</u> | [nazari:a] | z (ڙ) |

* Tanbihi: ingawa katika maandishi ya Kiswahili sauti dh na dh zinapanana, katika lugha ya Kiarabu sauti hizi mbili ni tofauti kabisa, ambazo ni d na z. Kwa mfano, neno *madarhi* katika lugha ya Kiarabu linatamkiwa [marađi], wakati neno *nadharia* katika lugha ya Kiarabu linatamkiwa [nazari:a].

Aidha sentensi zilizotumika katika utamkaji wa sauti zilizoorodheshwa hapo juu ni hizi zifuatazo:

1. wanafunzi wanapata maarifa mengi kutoka mtandao wa kimataifa.
2. watoto wabaya wanaleta aibu kubwa.
3. kwa heri Shehe, tutaonana kesho.
4. mtu huyu hana ruhusa ya kuendesha gari.
5. mwezi wa saumu ni Mwezi Mtukufu kwa Waislamu.
6. mwanafunzi yule amepata sifuri.
7. tuliiishi ghorofa ya nne.
8. tunapenda sana lugha ya Kiswahili.
9. mwizi alipelekwa mahakamani jana.
10. imetokea nini kuhusu hawala yako.
11. mtu yule ni wa kabilia gani?
12. watoto wanapenda kucheza wakati wote.
13. Waswahili wana tabia nzuri.
14. Kuegesha magari hapa ni hatari.
15. Mkulima amepanda figili.
16. Wanawake wanapendelea sana giligilani.
17. lafudhi ya Kiswahili ni tofauti na ya Kiarabu.
18. Katika utafiti wako umetumia nadharia gani?

Ili kuonyesha Matatizo yatokanayo na athari za utamkaji wa maneno yenyeye asili ya Kiarabu (yenye sauti ambazo hazimo katika Kiswahili). Hebu tuangalie matokeo ya utamkaji wa wanafunzi kama yanavyojidhirisha hapa chini:

Wanafunzi walipewa maneno na sentensi za kusoma, ili kujua matatizo ya athari za sauti za Kiarabu ambazo zimo katika maneno ya Kiswahili yenyeye asili ya Kiarabu. Hebu tuangalie matokeo ya utamkaji wao.

Athari ya sauti ئ (ع): Matokeo ya utamkaji wa maneno ya Kiswahili yenyeye asili ya Kiarabu yalionyesha kwamba wanafunzi wa asilimia ishirini tu ndio walioweza kuyatamka maneno hayo barabara. Wanafunzi wa asilimia themanini waliathiriwa sana na sauti hii. Kwa

mfano, neno [maarifa] walilitamka [maařifa].

Ama kuhusu sauti **kh** (خ): Wanafunzi wa asilimia thelathini ndio walioweza kuyatamka maneno yenyeye asili ya lugha ya Kiarabu sawasawa; yaani bila ya kuathiriwa na sauti hii, wengine wa asilimia sabini waliathiriwa sana na sauti hii. Kwa mfano, neno [ruhusa] walilitamka [ruxuša].

Sauti **š** (ص): Ni wanafunzi wa asilimia kumi tu ambaeo waliweza kuyatamka maneno hayo sawasawa. Wanafunzi wa asilimia tisini waliathiriwa katika utamakji wao nayo. Kwa mfano, neno [sabuni] walilitamka [šabuni].

Athari ya sauti ? (ء): Sauti hii siyo kama sauti zingine; yaani sauti hii haikuwa na athiri yoyote katika matamshi ya wanafunzi wote ishirini.

Athari ya sauti **q** (ق): Matokeo ya utamkaji yalionyesha kwamba wanafunzi wa asilimia sitini waliweza kuyatamka maneno barabara, na wanafunzi wa asilimia arbaini waliathiriwa na sauti **q** (ق). Kwa mfano, neno [kanuni] walilitamka [qanuni].

Athari ya sauti **d** (ض): Wanafunzi wa asilimia ishirini tu ambaeo waliweza kuyatamka maneno ya kiswahili yenyeye asili ya Kiarabu bila ya athari yoyote, wakati wanafunzi wa asilimia themanini waliathiriwa na sauti hii katika utamkaji wao. Kwa mfano, neno [maradhi] walilitamka [maradi].

Sauti **h** (ح): Inaonekana ni wanafunzi wa asilimia ishirini na tano tu ambaeo hawakuathiriwa nayo. Wanafunzi wa asilimia sabini na tano waliathiriwa na sauti **h** (ح). Kwa mfano, neno [hewala] walilitamka [hiwala].

Kuhusu sauti **t** (ط): Matokeo ya utamkaji wa wanafunzi wa asilimia themanini ambaeo hawakuathiriwa na sauti hiyo, wakati wa asilimia ishirini tu ambaeo waliathiriwa nayo.

Ama kuhusu sauti **z** (ڙ): ni wanafunzi wa asilimia kumi ambaeo hawakuathiriwa nayo. Athari ya sauti hii ilionekana wazi katika matamshi ya wanafunzi wa asilimia tisini ambaeo waliathiriwa na sauti hii. Kwa mfano, neno [lafudhi] walilitamka [lafuzi].

Matokeo ya athari za utamkaji wa maneno yenyeye asili ya Kiarabu (yenye sauti ambazo hazimo katika Kiswahili) kwa kundi hili yanaweza kuelezwaa kwa kutumia Jedwali lifuatalo:

| Sauti | Neno | Matamshi ya Kiswahili | Matamshi ya wanafunzi | | |
|------------|--------|-----------------------|-----------------------|------------|------------|
| | | | [ء / ئ] | [ماارِفَة] | [ماارِفَة] |
| | | | | 20 % | 80% |
| [kh / خ] | Ruhusa | [ruhusa] | [ruhusa] | [ruxuša] | Jumla |
| | | | | 30% | 70% |
| [š / ص] | Sabuni | [sabuni] | [sabuni] | [šabuni] | Jumla |
| | | | | 10% | 90% |
| [? / ء] | Swali | [swali] | [swali] | [sw?ali] | Jumla |
| | | | | 100% | 0% |
| [q / ق] | Kanuni | [kanuni] | [kanuni] | [qanuni] | Jumla |

| | | | | | |
|-------------|----------|------------|------------|------------|-------|
| | | | 60% | 40% | 100% |
| [d / (ض)] | Maradhi | [maradhi] | [maradhi] | [marađi] | Jumla |
| | | | 20% | 80% | 100% |
| [h / (ح)] | Hewala | [hewala] | [hewala] | [hiwala] | Jumla |
| | | | 25% | 75% | 100% |
| [t / (ط)] | Karatasi | [karatasi] | [karatasi] | [karatasi] | Jumla |
| | | | 80% | 2 0% | 100% |
| [z / (ظ)] | Lafudhi | [lafudhi] | [lafudhi] | [lufuzi] | Jumla |
| | | | 10% | 90% | 100% |

Matokeo ya utamkaji wa wanafunzi.

6.3 Makosa Yatokanayo na Utamkaji wa Mfuatano wa Irabu mbalimbali.

Katika Kiswahili irabu mbili tatu au zaidi zinaweza kupangiliwa katika kujenga maneno ya Kiswahili. Katika utafiti wa uwandani uliofanywa kwa kundi lililotajwa, wanafunzi walipewa maneno na sentensi zenye mfululizo wa irabu mbalimbali; yaani maneno yenye mfululizo wa irabu mbili, irabu tatu, irabu nne hadi tano. Hebu tuangalie maneno yaliyotumika katika zoezi hili:

1. Mwalimu ametoka saa sita.
2. Ninasoma Kiswahili kila siku.
3. Ninasikia njaa. Nilettee samaki tulio wavua jana.
4. Chuo kikuu cha Dar es salaam kinafundisha mafunzo mbalimbali.
5. Mwanamke huyu ana ua moja na yule ana maua matatu.
6. Waarabu bado hawajazoea kutamka sauti za ving'ong'o.
7. Watu wawili waliooana mwaka jana wanakaa pamoja.
8. Watu waliounganisha simu yangu wako hapa.
9. Ole woa wanafunzi watakaoiaibisha Libya.

Kutokana na utamkaji wa maneno na sentensi hizo yalijidhihirisha kama ifuatayo hapa chini:

Matokeo ya utamkaji wa maneno yenye mfuatano wa irabu mbili yalidhihirisha kwamba kati ya wanafunzi kumi na sita, wanafunzi kumi na wa nne waliweza kutamka maneno yenye mfululizo wa irabu mbili kwa usahihi; wanafunzi wawili tu ndio walioshindwa.

Mfululizo wa irabu tatu ultatanisha wanafunzi wa nane; yaani wanafunzi wa nane walishindwa kuyatamka maneno hayo.

Vilevile matokeo ya utamkaji wa mfululizo wa irabu nne yalionyesha kwamba mwanafunzi mmoja tu kati ya wanafunzi kumi na sita alishinda kuyatamka maneno yenye mfululizo wa namna hii.

Halikadhalika mfululizo wa irabu tano ultatanisha wanafunzi wote kumi na sita katika utamkaji wao.

Matokeo ya utamkaji wa maneno yenye mfululizo wa irabu mbalimbali kwa yanaweza kuelezwaa kwa kutumia Jedwali lifuatalo:

Aidha sentensi zilizotumika katika utamkaji wa sauti zilizoorodheshwa hapo juu ni hizi zifuatazo:

| Mfululizo wa irabu | Neno | Matamshi ya Kiswahili | Matokeo ya utamkaji wa wanafunzi | | |
|--------------------|-----------------|-----------------------|----------------------------------|----------|-------|
| | | | Kuweza | Kutoweza | Jumla |
| Irabu mbili | tia | [tia] | 90% | 10% | 100% |
| Irabu tatu | Maua | [maua] | 45% | 55% | 100% |
| Irabu nne | waliooana | [waliOana] | 5 | 95% | 100% |
| Irabu tano | watakaoiaibisha | [watakOiaibisha] | 0 | 100% | 100% |

Matokeo ya utamkaji wa wanafunzi.

7. HITIMISHO

Kutokana na tarifa zilizotolewa na zilizochuguzwa katika makala hii ya makosa ya kimatamshi yanayofanywa na wanafunzi wa Kiarabu wanapojifunza Kiswahili, wanafunzi wa Kiarabu wana makosa ya kimatamshi mbalimbali na kwa kiasi kubwa.

7.1 MATOKEO

1. Kutokana na taarifa na uchunguzi wa utamkaji wa sauti ambazo hupatikana katika lugha ya Kiswahili lakini hazimo katika lugha ya Kiarabu kama vile [ch, g, ng', ny, p, v] sauti hizo zinawatatanisha wanafunzi wa Kiarabu na
2. Kutokana na taarifa na uchunguzi wa utamkaji wa mfuatano wa irabu mbalimbali inaonekana wazi kwamba wanafunzi wa Kiarabu kwa jumla hawana matatizo kubwa ya kutamka maneno yenye irabu moja au mbili. Lakini

zinawaleta shida na makosa ya kutamka sauti hizo. Wanafunzi wa Kiarabu mara nyingi wanatumia sauti [b] badala ya sauti [p], sauti [f] badala ya sauti [v], sauti [sh] badala ya sauti [ch]. sauti [ng] badala ya sauti [ng']. sauti [i] badala ya sauti [e], lakini sauti [g na ny] ijapokuwa haimo katika lugha ya Kiarabu wanafunzi hawana matatizo ya kuzitamka sawaswa.

matatizo ya kutamka mfulilizo wa irabu inaonekana wazi na makosa yanajitekeza kwenye mfulilizo wa irabu tau, nne na tano.

3. Ama kuhusu utamkaji wa sauti za Kiarabu ambazo hazimo katika lugha ya Kiswahili (au ambazo zina asili ya Kiarabu), Kutokana na taarifa na uchunguzi inaonekana wazi kwamba wengi wa wanafunzi wa Kiarabu wana makosa na wameathiriwa na utamkaji wa lugha yao ya kwanza.

7.2 MAPENDEKEZO

Juu ya misingi ya matokeo ya uchunguzi wa matatizo ya kimatamshi yanayofanywa na wanafunzi wa Kiarabu wanapojifunza Kiswahili sanifu, tunatoa mapendekezo yafuatayo yanatolewa ili kupunguza matatizo hayo, na kuendeleza ufundishaji na ujifunzaji wa lugha Kiswahili.

- (a) Maabara Za lugha: Mojawapo ya zana muhimu katika kufundisha lugha za kigeni ni maabara ya lugha. Kutokana na utafiti huu tunapendekeza matumizi ya maabara za lugha. Wanafunzi wanapaswa kutumia maabara angalau mara tatu kwa wiki. Kanda zilizorekodiwa vizuri na kutayarishwa na wataalamu husika ndizo zitumike. Kwa kutumia maabara za lugha wanafunzi wanaweza kusikiliza, kuongea na kufanya mazoezi kadri wawezavyo.
- (b) Vielelezo: Vielelezo na matini zinazohusika lazima vizingatiwe na kutumiwa na walimu wa Kiswahili katika kufundisha lugha hii. Kila Mara walimu wajitahidi kueleza mambo yote kwa kutumia lugha ya Kiswahili badala ya kutumia lugha ya Kiarabu.
- (c) Kueleza Mahali pa Matamshi: Ufanuzi wa mahali pa matamshi ni hatua muhimu sana katika kuelezwa na kufanولي hasa kwa sauti ambazo hazimo katika lugha ya wanafunzi au sauti ambazo zimo katika lugha hizi mbili lakini zinatamkwa kwa namna tofauti.
- (d) Ujuzi wa walimu: Kutokana na taarifa na uchunguzi wa matatizo ya kimatamshi yanayowakumba wanafunzi wa Kiarabu na kuangalia ufundishaji wa Kiswahili, inaonekana kwamba walimu wengi hawana maarifa au sifa zinazostahili kufundisha lugha za kigeni. Inapendekezwa kwamba walimu wapewe mafunzo ya kutosha zaidi katika kuelewa fonolojia ya Kiarabu na Kiswahili pamoja na matatizo ya wanafunzi kuhusu kipengele hicho. Jukumu kubwa la walimu liwe ni kuwapatia wanafunzi maarifa na ujuzi wa matamshi ya kila sauti.
- (e) Mtaala mahsus i kwa wageni: Utayarishaji wa vitabu vya kufunzia lugha kwa wageni ni jambo muhimu sana (taz. Besha, 1983). Tunapendekeza kwamba wataalamu amba wanaandaa mtaala wa kufundisha wageni wazingatiwe fonolojia za lugha zote mbili, kiwango cha wanafunzi, mazingira, uhusiano, tofauti na athari za lugha ya awali juu ya wanafunzi hawa. Kuzingatia mambo hayo kutasaidia kujua lugha ya Kiswahili kwa upesi zaidi.
- (f) Mbinu na njia za kufundisha: Hizi zichaguliwe na waalimu kadiri ya malengo ya kozi ambazo zimekadiria kutosha uwezo na mahitaji yao.
- (g) Mazoezi: Kuongea na watu amba lugha yao ya awali ni ya Kiswahili, kuna faida kubwa katika kufanya mazoezi ya matamshi.
- (h) Kulinganisha na Kulinganua sauti za Kiswahili na za Kiarabu: Ni muhimu sana kujaribu kulinganisha na kulinganua sauti za Kiswahili na za Kiarabu ili kuonyesha tofauti zilizopo kati ya sauti za lugha hizi mbili; yaani kuonyesha ni sauti zipi zinaonekana kufanana, na zipi zinatofautiana; au zipi zinapatikana katika lugha moja lakini hazimo katika lugha

nyingine. Kutokana na hali hii wanafunzi wataweza kuona na kutafautisha sauti mbalimbali katika lugha hizo.

- (i) Nyimbo: Katika jumla ya jitihada za kuendeleza matamshi ya wanafunzi, hasa wageni wa lugha, tunapendekeza walimu watumie pia nyimbo katika kuwafundisha wanafunzi wao na kuwawezesha kucheza na sauti. Kwa kutumia njia hii wanafunzi watazoea kuzitamka sauti zote. Pamoja na hivi, sauti ambazo hazimo katika lugha yao ya awali wataweza kuzirudiarudia hadi wazee na kuweza kuzitamka bila shida.

8. MAREJEZO

Abdulkader, S. S. (1988)

صالح سليم عبد القادر الدلالة الصوتية في اللغة العربية منشورات جامعة سوهاج (1988)

Alhadidi , A. (1978)

على الحديدي مشاكل تعلم اللغة العربية لغير العرب القاهرة دار الكتب المصرية (1978).

Aniss, I. (1965) (1965)

ابراهيم انيس في الاتجاهات العربية مكتبة الطبعة الثالثة الأنجلو المصرية

Barkawi, A. (1984)

عبدالفتاح البركاوى مقدمة فى اصوات اللغة مؤسسة الرسالة الطبعة الثالثة

Besha, M.R. (1983) "Utayarishaji wa vitabu vya kufunzia wageni Kiswahili." *Makala za semina ya kimataifa ya waandaishaji wa Kiswahili .* (TUKI) uk. 60-76

Bosha, I (1993) *Taathiri za Kiarabu katika Kiswahili pamoja na Kamusi Thulathiya*, Dar es salaam University Press.

Bosha, I. (1994) Athari za Kiarabu katika Kiswahili sanifu. M.A Dissertation. University of Dar es salaam.

Guthrie, M. (1970) *Collected Papers on Bantu Linguistics*. Farnborough: Gregg. International Publishers.

Gumati, M.M. (1986)

محمد منصف القماطي الأصوات ووضائفها منشورات جامعة الفاتح كلية التربية

Haji, A.I. (1983) "Jinsi ya kuandaa somo la sarufi ya Kiswahili kwa wageni." *Makala za semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili .* (TUKI) uk.147-172

Heine, B. (1979) *A Typology of African languages : Based on the order of Meaningful Elements*. Deitrich Reimer.

IPA (1981) *International Alphonetic Association*, University college, gower street, London WCIE 6BT.

Kassulamemba, F.T (1977) Tanzanian Spoken English: Error Analysis of the Vowel system. M.A Dissertation. University of Dar es salaam.

Kihore, Y.M. (1984) "Kiswahili katika hati za Kiarabu." *Mulika Na.16* TUKI.

Kihore ,Y.M. (na wenzie) (2001) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili sanifu* , TUKI

Magoti ,A. (1980) "Ufundishaji wa Kifaransa kwa Watanzania: Mwingiliano wa mifumo ya vitamkwa vya Kiswahili na vya Kifaransa ". Unpublished paper.

Massamba, D.P (na wenzie) (2001) *Sarufi Miundo ya Kiswahili sanifu* , TUKI

Rawhia, K. (1984) *The problems encountered by English speakers in learning Arabic.* General publication of distribution company Tripoli.

TUKI (1990) *Kamus sanifu ya isimu na lugha.* DUP. Dar es salaam.